

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS – MAENDELEO YA VIJANA (OR–MV)

TANGAZO RASMI LA FURSA YA MKOPO WA MFUKO WA MAENDELEO YA VIJANA

Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umeanzishwa kwa lengo la kuwawezesha vijana kiuchumi kwa kuwapatia mitaji itakayowawezesha kuanzisha au kuendeleza shughuli mbalimbali za uzalishaji, biashara na utoaji wa huduma. Kupitia mpango huu, Serikali inalenga kuongeza ajira kwa vijana, kukuza ujasiriamali na kuchochea maendeleo ya uchumi wa Taifa.

Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana (OR–MV) inapenda kuwatangazia vijana wote nchini kuwa dirisha la kupokea maombi ya mkopo kupitia program ya Shilingi Bilioni 200 ahadi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalum limefunguliwa rasmi. Vijana wote wenye miradi au mawazo ya miradi wanakaribishwa kutuma maombi.

Sifa za mwombaji wa mkopo

Sifa zinazohitajika kwa waombaji kupata mkopo;

- i. Awe ni raia wa Tanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 mpaka 35;
- ii. Awe na nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au Namba ya NIDA;
- iii. Awe kwenye eneo linalotambuliwa na Mamlaka kwa ajili ya kufanyia biashara; mfano soko;
- iv. Awe mkazi wa eneo husika na awe na barua ya uthibitisho kutoka Serikali za Mitaa/Kijiji;
- v. Awe aidha mtu mmoja, kampuni changa au Kikundi cha Kijamii kilichosajiliwa kinachofanya shughuli ya kiuchumi;

- vi. Awe na andiko la mradi/biashara inayoombewa mkopo;na
- vii. Awe na akaunti ya benki au namba ya simu iliyosajiliwa kwa jina la mwombaji;

Namna ya kuomba Mkopo

Mwombaji wa mkopo atatakiwa kuwasilisha barua ya maombi ya mkopo ikibainisha masuala yafuatayo:

- i. Jina la kikundi au mwombaji;
- ii. Aina ya mradi unaopendekezwa;
- iii. Kiasi cha mkopo kinachohitajika; na
- iv. Mahali mradi utakapotekelwa.

Mwombaji atatakiwa kuambatisha Nyaraka zifuatazo wakati wa kuomba mkopo:

- i. Andiko la mradi lisilozidi kurasa tano (5);
- ii. Kitambulisho cha Taifa au Namba ya NIDA/ Kitambulisho cha Mpiga Kura;
- iii. Utambulisho wa Mlipa kodi (TIN);
- iv. Leseni ya biashara kwa biashara inayoendela;
- v. Barua ya utambulisho wa eneo la biashara kutoka kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa/Kijiji;
- vi. Picha mbili za mkopaji zilizopigwa ndani ya muda usiozidi miezi mitatu kabla ya maombi; na
- vii. Muhtasari wa kikao uliosainiwa na wanachama wa kikundi wenye ajenda ya maombi ya mkopo.

Mwisho wa Kupokea Maombi

Maombi yote yawasilishwe kabla ya tarehe 03 Aprili, 2026 kupitia barua pepe: mikopo@vijana.go.tz

Limetolewa leo tarehe 21 Machi, 2026 na:

**KATIBU MKUU
OFISI YA RAIS MAENDELEO YA VIJANA
S.L.P 2255
DODOMA**

Barua pepe: mikopo@vijana.go.tz